



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 17 Mei, 2022

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. MASWALI:

Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

162. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika ziara aliyofanya Makamu wa Pili wa Rais mwaka 2021, katika jimbo la Fuoni kwenye maeneo ya Mambosasa, bonde la Fuoni Jangamizini na Fuoni Kibondemzungu yanayoathirika na mvua na kupelekea kuundwa kamati ili kutoa mapendelekezo yatakayopunguza athari za mafuriko katika maeneo hayo.

Je, ni hatua zippi zilizochukuliwa katika maeneo ya Mambosasa, Fuoni Jangamizini na Fuoni Kibondeni.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

135. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Ni jambo jema kwamba Serikali imeridhia Sheria mpya ya Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa lengo la kuhakikisha kwamba Zanzibar inakuwa salama kutokana na athari za dawa za kulevyta. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wadau kwamba kufeli kwa sheria zilizopita kulisababishwa na

ukweli kwamba utekelezaji wake uliwbana zaidi wanyonge na kujihisi kuonewa.

- (a) Je, ni watu wangapi na wa ngazi gani katika biashara ya dawa za kulevyta walikamatwa, kuthibitika na kuhukumiwa kwa kesi za dawa za kulevyta katika miaka mitano iliyopita.
- (b) Je, ni watu wangapi na wa ngazi gani katika biashara ya dawa za kulevyta walikamatwa na kutothibitika na kuhukumiwa kwa kesi za dawa za kulevyta katika miaka mitano iliyopita.
- (c) Je, ni wangapi katika (a) na (b) walikuwa ni wageni na wangapi walikuwa ni Wazanzibari wakaazi.

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Viwanda:

153. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Miongoni mwa mambo yanayowakwamisha wawekezaji kuweza kutekeleza miradi yao mbali mbali ya kimaendeleo ni suala zima la ucheleweshaji wa "land transfer certificate".

- (a) Je, Wizara ina mkakati gani wa haraka wa kulitatua tatizo hili ili liondoke kabisa.
- (b) Je ni sababu zipi za msingi zinazopelekea ucheleweshaji huo na Je, Wizara yako ina mkakati gani wa kuiondoa kadha hii.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

110. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa muda mrefu Kituo cha Mafunzo ya Amali kilichopo Vitongoji kimekuwa na kilio cha kutokuwepo kwa uzio (fence) uliozunguka majengo ya kituo hicho. Na kwa kuwa tayari uzio umejengwa kwa takribani asilimia 80 kwa maana kuta za mashariki, magharibi na kaskazini ikibakia eneo la kusini ya majengo ya chuo hicho.

- (a) Ni sababu gani ya msingi iliyosababisha eneo la kusini la uzio wa kituo hicho usijengwe.

- (b) Ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa uzio huo.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

121. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, maliasili na Mifugo:

Kwa miaka mingi, kulikuwa na ukulima wa mpira katika eneo linalokatiza barabara ya Maziwani– Mtijuu iliyomo ndani ya jimbo la Pandani. Hata hivyo, inasikitisha kwamba wanajamii wa kijiji cha Maziwani ambao mashamba yao mengi yalichukuliwa na Serikali wakipewa ahadi nyingi za kimaendeleo zikiwemo ahadi za kutengenezewa barabara ya Maziwani–Mtijuu kutokana na mapato ya kilimo hicho. Hata hivyo, hadi sasa barabara hiyo imepuuzwa kabisa na Serikali imeshaachana na kilimo hicho katika eneo hilo.

- (a) Je, ni kiasi gani cha mapato ya Serikali yalitokana na zao la mpira ambalo mashamba yake yako sambamba na barabara hiyo.
- (b) Je, ni kiasi gani cha mapato ya Serikali yaliyotokana na zao la mpira yalielekezwa katika kuleta maendeleo ya eneo husika.
- (c) Je, ni kiasi gani cha mapato ya Serikali yaliyotokana na zao la mpira yalielekezwa katika kuitengeneza barabara hiyo.

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

93. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwa kuwa eneo la Chamanangwe ni eneo lililotengwa kwa ajili ya uwekezaji, na kwa kuwa hatua mbali mbali zilianza kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na uwekaji wa njia za ndani na miundombinu ya maji na umeme.

- (a) Je, Mradi uliokusudiwa kutekelezwa umekamilika
- (b) Je, ni tija gani iliyopatikana kwa wananchi na Serikali kwa ujumla juu ya uwekezaji huo.

II. **HOJA ZA SERIKALI:**

Waziri wa Afya:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
17 Mei, 2022.


(Raya Issa Mselleem)
KATIBU WA BARAZA